Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)



74. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w. ,** *Al-Jami'-ul-Saghir, J. 1 Uk. 14:*

*"Wafunzeni watoto wenu vitu vitatu: Mapenzi ya Mtume wenu, Mapenzi ya Ahlul-Bayt, usomaji wa Qur'an."*

75. **Amesema Al-Imam Ja'far as-Sadiq a.s.,** *Bihar al- Anwar* , *J. 74, uk. 354:*

*"Mtu yeyote ambaye hawezi kutufanyia wema wowote sisi Ahlul-Bayt basi wawafanyie mema wafuasi wetu walio wema; na yeyote yule asiyeweza kutuzuru, basi wanaweza kuwazuru wafuasi wetu walio wema ambavyo thawabu za kutuzuru sisi zitaandikiwa."*

76. **Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s.,** *Al-Kafi*, *J. 1,Uk. 187:*

*"Kwa kile kilicho bora kabisa kwa mja kumkaribia Allah swt ni utiifu kwake Allah swt, utiifu kwa Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w.. na utiifu kwa **ulil Amr**."*

Aliendelea kusema:

*"Mapenzi yetu* (*ya Ahlul-Bayt*) *ni Imani na chuki dhidi yetu ni kufr."*

77. **Amesema Al-Imam Ja'far as-Sadiq a.s.** *Bihar al- Anwar* , *J.27, Uk.91:*

*"Kwa hakika zipo daraja za ibada, lakini mapenzi yetu, Ahlul-Bayt, ni ibada iliyo bora kabisa."*

**Source URL:**
https://www.al-islam.org/hadith-za-mtume-s-na-ma-imamu-amiraly-m-h-datoo/mapenzi-ya-ahlul-bayt